**THE SUCCESS PATH EXAMINATION COUNCL (SPEC)**

**Paving the Way to Success**

**102/2**

# KISWAHILI

## LUGHA

**Karatasi ya 2**

**PRE-MOCK EXAMINATION 2026**

**MACHI 2025**

**Muda: Saa 2**

---

**Jina**: …………………………………………………. **Numbari ya Usajili** …………………

**Shule** ……………………………….………… **Mkondo**: ……………………………….

**Sahihi ya Mtahiniwa** …………………….…………… **Tarehe:** ………………………………..

**Maagizo**

(a) Andika jina lako na nambari yako ya Usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Andika jina ya shule kisha tia sahihi yako katika nafasi ulizoacha hapo juu.
(c) Jibu maswali **yote.**
(d) Maswali yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
**(g) Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.**
**(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |


©202 The Success Path Examination Council

**1. UFAHAMU** (Alama 15)

*Soma kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa kueleza chanzo au kiini cha mawasiliano na sote tunakubaliana kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo kwa jamii ya watu bila lugha ya mawasiliano yoyote ile.

Katika taifa lolote,huwepo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo zatika cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za:elimu, maandishi, siasa na biashara.Kwa mfano mataifa ya Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na za kikazi. Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za taifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kikabila. Lugha ya taifa ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile.Lugha hii huwa ndiyo kiungo cha kueneza umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kwa kuwa wao ni ndugu wa jamii moja kubwa, yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila.Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha vikundi hivi kilijitambulisha kama taifa huru.Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni na hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru,haja ya kuunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja lilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana.Kwa hivyo utamaduni wa taifa la Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila,desturi,imani na itikadi tofauti. Utamaduni humaanisha jumla ya amali na tabia za watu wa jamii fulani. Amali hizi zinafungamanisha fikira, ustaarabu, mila, taasisi na sanaa za aina zote za jamii inayohusika. Ili kujieneza na kujiimarisha,taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuwaunganisha watu wake wenye asili mbalimbali.Chombo hicho huwa ni lugha ambayo siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali pia ni njia muhimu sana ya kutawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa lenye lugha nyingi kama Kenya kwa mfano,lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na idadi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kueneza maongozi ya taifa, bendera ya taifa, ndicho kielelezo cha taifa lolote lile lililo huru. Lugha kama hiyo huvunja na hukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ni kielelezo cha fikira na hisia za binadamu.Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao kimaisha, falsafa na mawazo yao. Kwa ufupi lugha hutufahamisha namna akili za watu waizungumzayo ile lugha zinavyofikiri na kutafanya maazimio.Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa ilimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya jamii ihusikayo.Utamaduni wa jamii havitenganiki na lugha yake.


©202 The Success Path Examination Council

(a) Ni nini fasiri ya neno lugha? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Tofautisha baina ya lugha ya taifa na lugha ya kikazi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(c) Kwa nini lugha ya taifa huhitajika sana katika nchi kama Kenya? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(d) Taja kazi **tatu** kuu zinazotekelezwa na lugha ya taifa. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama 3)

(i) Haiyamkiniki:

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(ii) Amali na tabia za watu;

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(iii) Kielelezo:

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(iv) Muktadha wa maisha ya jamii:

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………


©202 The Success Path Examination Council

(f) Eleza majukumu mawili ya lugha kwa ujumla. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

**2. UFUPISHO** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatasho kisha ujibu maswali.*

Kwa kawaida, binadamu huishi kwa kutangamana na binadamu wenzake. Katika kutangamana huku, watu huathiriwa kitabia, kififikira, kimavazi na kimaisha kwa jumla. Watu wote katika jamii wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa na wenzao wa umri mmoja. Hata hivyo, walio katika hatari ya kuathiriwa zaidi na mahirimu wao ni vijana. Hali hii ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika au shinikizo-marika. Vijana huaminiana na kuthaminiana sana. Kwa sababu hiyo, ni rahisi sana kuingizwa katika mitego na wenzao. Isiaminiwe kuwa vijana pekee ndio wanaoathiriwa na shinikizo-rika. La hasha! Watu wazima pia huwafuata wenzao mithili ya bendera kufuata upepo. Mwenzake akinunua gari, yeye pia hukimbilia mkopo kununua gari la sampuli iyo hiyo bila kuwazia kima cha kibindo chake.

Wataalamu wa saikolojia husema kuwa kukabiliana na tatizo la shinikizo-rika si rahisi kwa sababu shinikizo-rika huleta mtafaruku wa kinafsi akilini mwa anayeathiriwa. Nafsi moja humshawishi kufuata wenzake huku nyingine ikimnasihi kuandamana upekee au ubinafsi wake. Shinikizo-rika huathiri sana mahitaji ya kisingi ya binadamu. Ikumbukwe kuwa mahitaji haya ya kimsingi ni ya kila mwanadamu, nayo ni kama vile kupata lishe, hewa safi, kupenda na kupendwa miongoni mwa mengine. Kila mtu hutaka kujihusisha na kundi la watu ambao watamfanya kuhisi kuthaminiwa na kukubalika. Kutokana na haja ya kutaka kukubalika, anayetaka kutambuliwa huridhia matakwa ya wenzake bila hata kuyawazia.

Shinikizo-rika hujittokeza kwa sura nyingi. Mathalani, vijana huwafanya wenzao kuona kuwa wana hatia wasipoafiki kutekeleza kama wanavyoshinikizwa. Kauli kama vile ‘tulifikiri wewe ni mmoja wetu’ au ‘usiposhirikiana nasi utakuwa umetuvunja moyo’ hutamalaki. Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kufanyiwa stihizai na wenzao na hata kutengwa. Vitisho hutolewa, wakati mwingine, na anayeshinikiswa akidinda, mabavu hutumika.

Ni muhimu kwa watu, hasa vijana, kufahamu kuwa shinikizo-rika lipo na wanapokabiliwa na tatizo hilo, watambue kuwa wana haki ya kusimama kidete kutetea msimamo wao dhidi ya wenzao. Kumbuka, baridi huwazizima kondoo kwa namna tofauti.

Kama njia moja ya kukabiliana na shinikizo-rika, wanasaikolojia wanapendekeza watu kujiamini na kuelewa kwamba wana haki ya kuwa tofauti na kuwa na upekee wao. Mtu anapojiamini na kushikilia msimamo wake, anaweza kujiepusha na madhara yatokanayo na shinikizo-rika. Asiyejiamini huwa mwepesi sana wa kuingizwa katika lindi la mashaka na wenzake.

 ©202 The Success Path Examination Council

(a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa **maneno 40**. (alama 9)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**Nakala Safi**

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**(b)** Fupisha mambo muhimu ambayo mwandishi amezingatia katika aya tatu za mwisho kwa maneno 30. (alama 6)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**Nakala Safi**

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………..


©202 The Success Path Examination Council

**3. MATUMIZI YA LUGHA** (Aama 40)

(a) Tofautisha kati ya: (i) / e / (ii) / u / (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Onyesha **muundo** wa **silabi** ya kwanza katika maneno yafuatayo: (alama 2)

(i) Nyakua

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(ii) Chura

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

(c) Tunga sentensi kwa kutumia kibadala cha kiasi jumla. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(d) Changanua sentensi ifuatao kwa kutumia **jedwali**. (alama 4)

Mkongojo mrefu sana ulioletewa babu utauzwa na fundi mcheshi.

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

(e) Andika **kinyume** cha sentensi ifuatayo:

Mtoto msichana anathema dawa. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

(f) Kanusha: (alama 2)

Nikimpiku masomoni nitatuzwa zawadi.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(g) Andika katika usemi halisi. (alama 3)

Chifu wetu alitwambia kuwa watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)

(i) (-la) (kauli tendeshea)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Toa (tendeka)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(j) Eleza matumizi ya alama zifuatazo za uakifishi. (alama 2)

**(i) !**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**(ii) ?**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(k) Bainisha mofimu **–Li-** katika tungo hili. (alama 3)

Alivyolikimbilia

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(l) Tunga sentensi moja yenye shamirisho hizi. (alama 3)

(i) Kipozi

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Kitondo

(iii) Ala

(m) Ainisha vishazi. (alama 2)

Mhamiaji haramu aliyeshikwa amefikishwa mahakamani.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(n) Andika katika wingi karibu. (alama 2)

Mtu yuyo huyo aliubeba mzigo uo huo licha ya kukanywa.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(o) Andika sentensi ifuatayo katika watati ujao timilifu. (alama 2)

Mbunge alitawazwa kabla ya mpinzani wake kufika.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(p) Andika kwa wastani. (alama 1)

Magoma haya yatachezwa wanjani.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(q) Taja na utoe mifano, matumizi mawili ya kiimbo. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

(r) Eleza maana mbili za sentensi. (alama 2)

Nenda ukaniletee mbuzi.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

**4. ISIMU JAMII:** **(Alama 10)**

(a) Ali: Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!
Ebo: Mimi … ni … afande ni Ebo
Ali: Unatoka wapi sa ii? Hapa hakuna sheria?
Ebo: Samahani mkubwa. Mimi niku…
Ali: Mkubwa wa nani? Wakubwa wako ofisini.
Ebo: Pole mzee.
Ali: Mzee gani? Hii mtu lazima niiwekwa store. Yaani self-contained. Toa viatu.
Ebo: Tafadhali Bwana Askari, nilichelewa …
Ali: Mimi sitaki hadithi! Hizo pelekea nyanya yako, eh. Fanya haraka!
Ebo: Naomba mkubwa …
Ali: Hapa si kanisani. Unaomba! Hata …

Fafanua sifa tano za sajili hii. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimu jamii. (alama 5)

(i) Lugha ya taifa.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

(ii) Lugha ya ishara

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

 ©202 The Success Path Examination Council

(iii) Lugha mwiko

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(iv) Sajili za lugha.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(v) Uchanganyaji msimbo.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………


©202 The Success Path Examination Council